

Please check the examination details below before entering your candidate information

Candidate surname

Other names

**Pearson Edexcel
International GCSE**

Centre Number

--	--	--	--	--

Candidate Number

--	--	--	--	--

Thursday 23 May 2019

Morning (Time: 2 hours 15 minutes)

Paper Reference **4SW1/01**

Swahili

Paper 1 : Reading, Writing and Translation

You do not need any other materials.

Total Marks

Instructions

- Use **black** ink or ball-point pen.
- **Fill in the boxes** at the top of this page with your name, centre number and candidate number.
- There are **three** sections you must answer:
 - Section A Questions 1–4
 - Section B Questions 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c)
 - Section C Question 7.
- Answer the questions in the spaces provided
 - *there may be more space than you need.*
- You must **not** use a dictionary.

Information

- The total mark for this paper is 80.
- The marks for **each** question are shown in brackets
 - *use this as a guide as to how much time to spend on each question.*

Advice

- Read each question carefully before you start to answer it.
- Check your answers if you have time at the end.

Turn over ►

P58205A

©2019 Pearson Education Ltd.

1/1/1/



Pearson

SECTION A: READING

Answer ALL questions.

Write your answers in the spaces provided.

Multiple-choice questions must be answered with a cross ☒. If you change your mind about an answer, put a line through the box ☒ and then mark your new answer with a cross ☒. Open-response questions do not have to be written in full sentences and you may respond using single words or phrases.

- 1 Malizia sentensi zifuatazo kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Weka alama sahihi kwenye kila kisanduku.

Hoteli ya Sarova

Hoteli ya Sarova iliyopo Mombasa ni mahali pazuri sana kwa familia zenye watoto wadogo wenye hamu ya kuenda likizo kando ya bahari. Ni hoteli ya kisasa yenye vyumba vinavyoangalia bahari. Wazazi wengi hupenda kupumzika kwenye vibaraza vya vyumba huku wakisoma vitabu.

Kwa watoto kuna mengi ya kufanya. Wanaweza kufurahia sanaa na ufundi ndani ya hoteli au wanaweza kuenda nje ili kucheza. Wengi hupendelea soka ya ufukweni. Watoto wanaweza kutumia mojawapo ya mabwawa matano ya kuogelea yaliyojengwa kwenye uwanja wa hoteli. Kila bwawa lina waokozi wawili wa majini ambao wameajiriwa kwa ajili ya kulinda.

Kuna migahawa minne. Familia nyingi hupendelea ule wenye vyakula maalumu kwa watoto ili waweze kujipakulia wenyewe.

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



- A** kazi **B** pendekezo **C** bwawa **D** maonyesho
E vitabu **F** starehe **G** barazani **H** mgahawani
I masomo **J** bahari **K** Mombasa **L** shughuli
M mpya

Example:	Hoteli ipo...	K
1 (a)	Hoteli ni... kwa familia zenye watoto wadogo.	
1 (b)	Kutoka kila chumba unaweza kuiona...	
1 (c)	Kusoma ni... kwa wazazi.	
1 (d)	Watoto wanaweza kufurahia uwingi wa...	
1 (e)	Bwawa ni mahali pa... kwa waokozi wa majini.	
1 (f)	... watoto huchagua wanachotaka kula.	

(Total for Question 1 = 6 marks)

DO NOT WRITE IN THIS AREA



2 Weka alama katika visanduku 10 vilivyo sahihi. Sentensi nyingine au watu wengine wanaweza kuwa na alama zaidi ya moja au bila alama yoyote.

Simu ya mkononi

Magati




Mimi ninaipenda simu ya mkononi ambayo nimekuwa nayo tangu shule ya msingi. Napenda kutazama mitandao ya kijamii na pia kupiga picha. Sipendi mtu atazame simu yangu ya mkononi kwani ninaitumia kuandika kumbukumbu zangu za siri.

Nambua



Nilikuwa na hamu sana ya kuwa na simu ya mkononi hivyo nimefurahi kuipata. Wazazi wangu walininunulia nilipoanza shule ya sekondari kwani ipo mbali na nyumbani kwetu hivyo iliwawezesha kuwasiliana na mimi na kujua sipo hatarini. Ninaporudi nyumbani ninaruhusiwa kuitumia kwa saa moja tu. Ninavutiwa na mitandao ya kijamii.

Baraka



Hivi sasa mimi naona simu ya mkononi kuwa kero lakini nilipokuwa shule ya msingi nilikuwa napenda kuchezea simu ya kaka yangu mkubwa. Wazazi waliponipa simu yangu ya mkononi sikujishughulisha na mitandao ya kijamii, bado ninapendelea michezo. Mara nyingi mimi husahau simu yangu ilipo.

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



		Magati	Nambua	Baraka
Mfano:	Ninapenda kuwa na simu ya mkono.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
A	Wazazi wangu wameninunulia simu.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
B	Nimetumia simu ya mkono nilipokuwa shule ya msingi.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
C	Ninapenda kutazama mitandao ya kijamii.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
D	Sipendi watu kusoma ninachoandika simuni.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
E	Nina kikomo cha muda wa matumizi ya simu.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
F	Sijali sana simu yangu.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
G	Nimepewa simu kwa usalama wangu.	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>

(Total for Question 2 = 10 marks)



- 3 Soma makala kuhusu Kahawa. Malizia taarifa kwa kutumia namba au maneno kwa **Kiswahili**.

Kahawa

Kahawa ni kinywaji ambacho watu wengi duniani kote hukipenda. Hunywewa hasa mikahawani na majumbani. Katika kisiwa cha Pemba, ni desturi kwa watu kukusanyika kwenye vibaraza na kujiburudisha kwa kunywa kahawa ya moto kutoka kwenye vikombe vidogo vya duara.

Mzee Habibu ni mwuzaji wa kahawa. Yeye hununua mahitaji yake kama matunda ya kahawa, viungo na sukari kila wiki. Pia hutayarisha vitafunio vitamu kama kashata na halua. Mzee Habibu hapendi kahawa ya vikopo kutoka madukani. Yeye huenda moja kwa moja kwa wakulima wenyewe na kuyanunua matunda haya yenye rangi nyekundu. Mti wa kahawa huchukua miaka mitatu kutoa matunda kwa mara ya kwanza. Mzee Habibu huyakausha kwa kuyaanika juani na pia kuyachoma. Baadaye huyasaga kwenye kinu na kuyachanganya na viungo kama tangawizi.

Mchanganyiko huu huchemshwa na kuwa na ladha ya kipekee. Harufu yake huwavutia wateja kuendelea kuinywa zaidi.

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

Mfano: Kahawa ni: kinywaji

- (a) Duniani kahawa hunywewa: na (2)
- (b) Kisiwani kahawa hunywewa: (1)
- (c) Chombo cha kunywa kahawa: (1)
- (d) Kazi ya Mzee Habibu: (1)
- (e) Rangi ya matunda ya kahawa: (1)
- (f) Muda kwa mkahawa kuchanua mwanzoni: (1)
- (g) Njia za kukausha kahawa: na (2)
- (h) Mchanganyiko una kahawa na: (1)
- (i) Wateja huvutiwa na: na (2)

(Total for Question 3 = 12 marks)



- 4 Soma habari ifuatayo kutoka kitabu kitiwacho **Mbali na Nyumbani**, kilichoandikwa na Adam Shafi.

Adam na familia yake

Ninaitwa Adam. Siku moja, tulikuwa tumekaa ukumbini kwenye nyumba yangu ya vyumba viwili iliyopo mjini Dar es Salaam. Ukumbi wa nyumba yangu ulikuwa umepambika vizuri kwani mke wangu, Fatma, ni hodari wa kuipanga nyumba.

Mimi, mke wangu Fatma na watoto wangu Shafi na Laila tulijistarehesha kwa kula keki, visheti na biskuti. Tulikuwa tukisherehekea siku ya kuzaliwa Shafi, aliyekuwa akitimiza miaka ishirini na moja. Ukumbini palikuwa pamejaa muziki tulioufungulia kwa sauti ndogo. Nilimtaja Shafi, nikamweleza kwamba nilipokuwa na miaka ishirini na moja kama alivyo yeye siku ile, sikuwa kama yeye. Nikamwonesha picha yangu nilipokuwa mwanafunzi wa chuo kikuu.

Aliitazama kwa makini sana na kuniuliza, "baba mbona pale unaonekana umekonda, hali yako dhaifu?"

"Mwanangu," nilimwambia, "Ujanani mwangu, tofauti na wewe, akili yangu haikuwa katika starehe za maisha mazuri. Pia mimi nilipenda kusoma. Kila siku nikiwaza lini nitaingia chuo. Basi mimi na rafiki yangu mmoja tulikuwa na ndoto kwamba tutasafiri kwa jahazi mpaka Kuwait. Huko tutafanya kazi na kukusanya pesa za kutosha halafu tutaishi maisha mazuri."

Jibu maswali kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Si lazima kuandika sentensi kamili.

- (a) Adam anaishi mji gani? (1)

- (b) Adam ana hisia gani kwa Fatma? (1)

- (c) Tunajuaje kwamba sherehe ya kuzaliwa kwa Shafi ilikuwa ndogo? (1)

- (d) Walifanya nini kusherehekea sikukuu ya kuzaliwa kwa Shafi?
Toa maelezo **mawili**. (2)



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(e) Picha inadokeza nini kuhusu maisha ya zamani ya Adam?

(1)

(f) Tofautisha mawazo ya Adam na Shafi walipokuwa na miaka ishirini na moja.
Toa maelezo **mawili**.

(2)

(g) Adam alikuwa na mipango gani ujanani mwake?
Toa maelezo **mawili**.

(2)

(Total for Question 4 = 10 marks)

TOTAL FOR SECTION A = 38 MARKS



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

(Total for Question 5 = 12 marks)



6 Chagua **moja** kati ya maswali matatu yafuatayo na andika maneno takribani 130 kwa **Kiswahili**.

Chaguo 1

(a)



Andika makala kupendekeza nchi ambapo kombe la dunia lingeweza kufanyika. Ni lazima uandike kuhusu:

- Sababu za kuchagua nchi hiyo
- Nafasi ya mpira wa mguu katika jamii
- Mawazo yako binafsi.

(20)

Chaguo 2

(b)

Nimesikia umerudi kutoka likizo uliyokwenda na familia yako. Tafadhali niambie ilikuwaje!

Rafikiyo,

Zenaida

Jibu kwa kutumia barua pepe. Ni lazima uandike kuhusu:

- Umuhimu wa likizo
- Matukio wakati wa likizo
- Mipango yako kwa mwaka ujao.

(20)



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

Handwriting practice area with 20 horizontal dotted lines.

(Total for Question 6 = 20 marks)

TOTAL FOR SECTION B = 32 MARKS



DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

DO NOT WRITE IN THIS AREA

BLANK PAGE

Source information

Question 2

- © skyNext/Getty Images
- © Steve Debenport/Getty Images
- © monkeybusinessimages/Getty Images

Question 6

- © spfdigital/Getty Images

